# KIBURI CHAPONZA KICHWA

## Hadithi ya watoto



ISBN 978-9976-5-7131-8

# MWANAWETU MMUNI

Hakimiliki © Mwanawetu Mmuni

*Mwanawetu Mmuni*
*P. O Box 90,*
Mtwara - Tanzania

© 2021

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi.

# Kiburi chaponza kichwa

Shule ya msingi Kichangani iliyopo mkoani Morogoro ilikuwa na wanafunzi wenye nidhamu sana. Wasingelimwona mgeni au mtu mzima yeyote anapita karibu yao bila ya kumsalimia au kumpokea mzigo alioubeba.

Siku moja wanafunzi wa darasa la Awali, walimuona Mwalimu wao anaelekea darasani kwao akitokea ofisi kuu. Walimkimbilia na kumpokea mizigo yake. Mwalimu Maimasa alibeba vitabu, kapu lenye chai na visheti. Kapu la visheti lilibebwa na Kuda. Harufu nzuri ya chakula ilifanya tumbo la Kuda liungurume kama simba; "ngruuuu!" Alitamani kuomba apewe angalau visheti vichache ili atulize njaa yake au aibe na kuvificha kwenye sare ya shule aliyoivaa. Lakini alikumbuka maneno ya mama yake kuwa, "ni tabia mbaya kutamani kitu cha mtu." Hivyo alivumilia hadi alipofikisha kapu ofisini bila kuiba kisheti hata kimoja. Watoto

waliweka mizigo ya Mwalimu wao ofisini na wao waliingia darasani.

Baada ya dakika chache kupita, Mwalimu Maimasa aliingia darasani akiwa amebeba lile kapu la visheki na sasa likiwa lipo wazi. Watoto alifurahia na kuruka ruka sababu walijua, hiyo itakuwa ni zawadi yao.

**Mwalimu**: Watoto hamjambo?

**Wanafunzi**: Hatujambo, Shikamo Mwalimu!

**Mwalimu**: Marahaba watoto wazuri, kaeni…!

Watoto walisimama kwa heshima pindi alipoingia Mwalimu darasani. Baada ya salamu, Mwalimu aliwaruhusu wakae.

Mwalimu Maimasa anapenda kuimba nyimbo pamoja na kutamba hadithi. Ni desturi yake kuanzisha wimbo kabla ya kutambulisha mada ya siku hiyo.  Wimbo uliimbwa hivi;

*Mabata madogo madogo, yanaogelea! Yanaogelea!*
*Katika shamba zuri la bustani.*

*Wanapenda kutembea bila viatu! Bila viatu!*
*Katika shamba zuri la bustani.*

*Wanapenda kulia kwa kwa kwa kwaaa! Kwa kwa kwa kwaaa!*
*Katika shamba zuri la bustani.*

Sauti nzuri za watoto ziliwavutia ndege na vipepeo kusogea karibu. Ndege walifika na kusimama madirishani, walianza kuimba wakigeza sauti za watoto. Walipomaliza kuimba wimbo wao vizuri, watoto walishangilia na ndege waliruka na kuondoka. Kumbe nje ya darasa kulikuwa linapita kundi kubwa la mifugo kama vile mbuzi, ng'ombe, kondoo, punda na mbwa. Mifugo hiyo ilikuwa inachungwa kuelekea malishoni na waliposikia sauti za

watoto wanavyoimba wimbo vizuri, walisimama kusikiliza.

Wanafunzi walishangaa alipoona tukio hilo. Hivyo Mwalimu Maimasa aliwaambia watoto kuwa atasimulia hadithi tamu kuhusu kisa cha ng'ombe na mbuzi kiburi walivyosababisha watu kuanza kula nyama.

Mwalimu aligawa visheti na maziwa kwa wanafunzi wote. Wakala na kushiba. Kuda alikumbuka jinsi alivyotamani kuiba visheti. Alijisemea, "kweli haraka haraka haina baraka. Ningeiba visheti vyetu. Ona sasa, tumepewa sote bila kuomba! Na aliyehitaji nyongeza amepewa pia. Kweli Mama yangu ni mtu mwenye busara sana.

**Mwalimu**: Watoto wazuri, mpo tayari kwa hadithi?

**Wanafunzi**: Ndiyooooo!

**Mwalimu**: Sawa. Twendeni bustanini.

*Watoto walitoka nje wakitimua mbio ili kuwahi nafasi iliyo karibu na mtambaji.*



**Mwalimu**: Paukwa!

**Wanafunzi**: Pakawa…..!

**Mwalimu**: Hapo zamani za kale….!


**Wanafunzi**: Eeeeeh!

**Mwalimu**: Binadamu alikuwa anafuga wanyama kama vile mbuzi, ng'ombe, punda, paka na mbwa kwa lengo la kusaidia shughuli mbalimbali za nyumbani na shambani. Sio kwa ajili ya chakula au biashara kama ilivyo sasa.



*Watoto walitulia tuliii! Wakisikiliza kwa makini. Mwalimu aliendelea;*

**Mwalimu**: Kama mjuavyo penye wengi hapakosi mengi na kwenye msafara wa mamba na kenge wamo. Miongoni mwa ng'ombe na mbuzi walioishi zama hizo, kulikuwepo na ndama wawili wenye kiburi. Ndama moja alikuwa ng'ombe na mwingine ni mbuzi.



Ndama hawa walimsumbua sana mchunga pindi walipokwenda machungani. Kila walipofika huko ilikuwa desturi yao kutoroka na kujificha vichakani. Siku za mwanzo, mchunga

alitaharuki kuwatafuta ndama hao wachanga akihofia wataliwa na fisi. Lakini kila siku zilipozidi kwenda, mchunga alichoshwa na tabia hiyo na kuamua kuwafundisha adabu. Alianza na zoezi la kuwafunga kamba shingoni kila waendapo machungani. Haikuwa tiba hivyo kuamua kuwachapa mijeledi kila wanapotia fujo.

Mijeredi na masemango viliwafanya ndama hao wawili waone wananyanyaswa. Walipanga njama yakutoroka ili wawe huru na usiku moja wakiwa wazazi wao wamelala walitoroka.

Kwa kuwa kulikuwa hakuna zizi wala ngome ya kuwazuia kutoka eneo hilo, ilikuwa rahisi kufanikiwa kutoroka.

Usiku huo mama ng’ombe mwenye kiburi na mama mbuzi mwenye kiburi, walilia sana baada ya kuwakosa watoto wao. Kulikuwa na kelele; Meee! Meee! Mooo! Mooo!

Mkulima alitoka nje ili kuchunguza kama mifugo yake imevamiwa na wanyama wakali wa porini. Wanyama wala mifugo ni simba, chui na fisi. Lakini hakukuwepo na hatari yeyote. Mazingira yalionesha kuwa salama. Hivyo mkulima alirudi ndani na masikio alitia pamba ili kuendelea kulala usingizi.

Asubuhi mapema, mkulima alikwenda kukagua shamba. Njiani alisikia mayowe, haoooo! haooo! Piga haooo!

Mkulima alisimama ili kujiridhisha kama hakuna tatizo. Ghafla aliwaona watu wanawakimbiza ng'ombe na mbuzi.





Kwa haraka haraka mkulima hakuweza kutambua kama ni mifugo yake hadi pale ndama walipofika miguuni mwake kujisalimisha.

Mkulima aliwatuliza wakulima wenzake waliobeba rungu, panga na mijeledi. Walikubali kutuliza munkari endapo watakubaliwa matakwa yao. Walidai kulipwa fidia kwa sababu ndama wameharibu mazao shambani. Ili kuondoa ngoma juani, mkulima alikubali kulipa.

Baada ya dakika chache kupita na watatu hao kuanza kushika njia; kulitokea mtu mmoja mwenye hasira aliyeita Mayula. Alichohitaji ni kupewa ndama ili achinje ndipo aridhike. Tayari mkononi alishika kisu kikubwa na kikali kilichomeremeta kama tumba. Azma yake ni kuwaua kwa sababu wametia kinyesi katika eneo lake analofanyia ibada. Kusikia vile, wahenga walishirikiani kumpoza mtu huyo aliyejinasibu kufanya ibada chini ya mti. Alisema; “ninamheshimu sana mungu wangu, sasa kwanini ndama wako waje kutia kinyesi?

Nikiwachinja, nadhani mungu ataridhika na kunisamehe.”

Ndama walianza kulia; Moooo! Meeee! Sababu walijua huo utakuwa mwisho wao wakuishi hapa duniani. hawatawaona mama zao, hakuna nyonyo, wala kuchenza kimbuzimbuzi!

Ndama walitazamana na kulia tena kwa uchungu; Mooo! Mooo! Meee! Meee!

Wakulima waliwahurumia ndama. Walijua walitenda makosa hayo kwa sababu ya udogo wao. Kwa kuwa ni kosa la kwanza, wanastahili kusamehewa ili waweze kujirekabisha.

Walimwambia mmiliki wa ndama ampe vipande vya dhahabu Mayula ili kukomboa mifugo yake. Mkulima alikubali kulipa lakini Mayula alikataa katakata kupokea vipande vya dhahabu. Dhima yake ni kuchinja wanyama hao, basi!

Mayula alisema;

“Ninyi mmeharibiwa mazao hivyo ni rahisi kurudishiwa mazao mengine, vipi kuhusu mimi

niliyechafuliwa bu..bu…buruji yangu kwa kinyesi?"

Watu wote walicheka na kumuuliza;

"Buruji? Wewe si umesema unafanyia ibada chini ya mti?"

"Tatizo hamjui nimeumia kiasi gani?" Machozi yalimlengalenga.

Mtu huyo aliinua tena kisu na kutaka kumchoma mbuzi. ndipo kijana mmoja aitwaye Nuru ambaye watu wengi humdharau kutokana na kakosa elimu. Yeye hajasoma hata darasa moja! Alipomsogelea Mayula, watu walianza kumzomea na kumsukuma; "huyooooo! Washindwe kuamua watu wenye elimu zao halafu utaweze wewe mbumbumbu?"

"Maajabu haya!" alisikika mama mmoja.

Nuru alipiga moyo konde na kujigeuza mwamuzi wa shauri hilo. Alianza kumtuliza Mayula kwa kumkumbusha kusamehe na kumuuliza swali;

“Endapo mtoto wako angelikuwa ndiye aliyefanya uharibifu huo kwa kukunyea kwenye mkono. Je, ungeliukata mkono au ungelimchinja mtoto?” Mayula alikosa jibu na kukubali kusamehe. Nuru alimgeukia Mkulima na kumwambia aenda kufanya usafi sehemu iliyochafuliwa.

Watu wote walishangilia; Nuru! Nuru! Na huo ukawa mwisho wakuitwa mbumbumbu. Watu walitawanyika na mkulima alitimiza ahadi yake ya kufanya usafi na kulipa fidia.

Mkulima aliwasamehe ndama wenye kiburi lakini tayari walishajitia doa. Kila walilolifanya lilionekana lina dosari. Kila aliyekosea, hakufuatiliwa bali lawama zote ziliwaangukia wao. Wizi wa mboga ni wao! Uharibifu wa mazao wafanye ngedere lakini walionekana wao! Kelele wapige punda lakini wataonekana wao! Muda wowote inapotokea hitilafu mkulima husema; “Ndama wenye kiburi hao, unadhani kuna mwingine?”

Mwishowe mkulima aliamua kujenga zizi ili kuepusha shari na kulipa madeni kila leo. Mara nyingine walisingiziwa na kubambikiwa makosa. Zizi lilikuwa mwarobaini wa watoro hao pamoja na wahujumu.

Mkulima alifurahi kuona ametatua tatizo kumbe alianzisha ugomvi wa ndani kwa ndani baina ya mifugo hiyo. Mifugo wapole na wenye nidhamu walichukia kifungo bila makosa. Lawama ziliongezeka kwa ndama wenye kiburi na kuanza kuchukiwa  na wazazi wao pamoja na wamyama wengine.



Mazingira haya yalipelekea ndama wenye kiburi kupewa adhabu mara kwa mara. Miaka ilipita bila kutoroka ingawa kiburi kiliendelea na kuwa ng'ombe na mbuzi wakubwa wenye kiburi.

Mkulima alibadilisha wachunga kila huchao! Leo huyu! kesho yule! Ilimradi tafrani. Lakini mkulima aliendelea kutokata tamaa na kuwafuga kwa kuwa hakuwa na mtu wakumtupia. Watu wengi walimtweza wakimwambia, "anawadekeza! Anawachekea! Anawatuma kufanya uharibifu na maneno mengine ya karaha.

Mkulima aliwaonya ng'ombe na mbuzi kiburi waweze kubadilika, bila mafanikio. Aliwaambia, "asiyesikia la mkuu huvunjika guu."

Siku moja wakiwa malishoni waliamua kutoroka tena ili wakaanze maisha mapya. Walisema; "tumeshakuwa wakubwa sasa tunahitaji kuwa huru. Tukitoka hapa jela tutakuwa hatufungiwi kwenye zizi tena!

Tutakula na kulala tupendapo! Tutakwenda kila mahali kwa muda tunaotaka! Tutakuwa na marafiki wengi kadiri tutakavyoona inafaa! Hatutanyanyaswa wala kuchapwa mijeledi! hatutatumwa kazi! Tuondokeeeee!”



Waliwashawishi wanyama wengine ili watoroke pamoja lakini njama yao ovu iligonga mwamba. Waliondoka peke yao.

Mkulima alipewa taarifa ya utoro wao. Alisema, “asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Watarudi wenyewe! Wala hasitokee mtu yeyote wakuwafuatilia!”

Baada ya wiki moja kupita, mkulima alipokea wito toka ofisi ya Mtendaji kata. Alitii wito huo. Alipofika ofisini, kabla ya salamu alikaribishwa na harufu ya damu, inayovuja toka kwenye mwili wa mbuzi na ng’ombe kiburi.

Wananchi wamefikisha shauri lao katika ofisi hiyo kwa kuwa mifugo hiyo imefanya uharibifu katika mashamba yao.

Mbuzi alikuwa anamlaumu ng’ombe kuwa ndiye aliyekula mahindi na mpunga wa wakulima. Kwa sababu yeye aliishia kula majani pekee. Mbuzi hakujua mahindi na mpunga unaozungumziwa sio punje bali ni mimea ya mahindi na mpunga.



Kama kawaida ya Mkulima alilipishwa fidia na kutozwa faini. Alichukua majeruhi wake na kurudi nao nyumbani.

Wakiwa njiani, walikutana na vijana watatu toka vijiji vya mbali. Walimuuliza mkulima sababu ya mifugo yake kupata majeraha makubwa kiasi hicho. Mkulima alijitetea kwa kusimulia mkasa mzima. Vijana hao walimshawishi mkulima kuwauza ng’ombe na mbuzi hao kwa kuwa wao wanadawa yakutibu majeraha ya mifugo. Hivyo watawatibu na kupona kabisa. Ng’ombe na mbuzi kiburi walifurahi sana na kusahau maumivu ya majeraha yao pamoja na njaa waliyonayo, baada ya kufungiwa zaidi ya siku mbili akisubiriwa mmiliki wao kuwakomboa.

Mkulima alikubali kuuza wanyama hayo na kurudi nyumbani akiwa na fedha alizotumia kufutia machozi yaliyosababishwa na mfululizo wa madeni.

Ng'ombe na mbuzi kiburi walipofika makazi mapya yanayomilikiwa na tajiri mwenye kasri kubwa. Walipokelewa na kupelekwa bandani. Wakiwa wanapata chakula na maji, waliwaona watu wanajaa katika eneo hilo na kuwa wengi.

Badala ya kutibiwa majeraha, ng'ombe kiburi na mbuzi kiburi walichinjwa na kuliwa nyama kwenye sherehe ya ukoo. Huo ukawa mwisho wa kiburi chao!

Tangu siku hiyo wafugaji wamekuwa wanauza ng'ombe na mbuzi na wafanyabiashara huchinja mifugo hiyo na kutumiwa kama kitoweo. Kiburi cha ng'ombe na mbuzi kiliwaponza na ndugu zao. Wahenga husema, "kila mchuma janga, hula na wakwao". Ng'ombe na mbuzi hao walisababisha wenzao kuchinjwa hata wale wenye nidhamu na wapole.

***

Mwalimu Maimasa alimaliza kusimulia hadithi yake.

Watoto walifurahi sana na kujiahidi kutokuwa na tabia mbaya ya kiburi kama ya ndama wenye kiburi.

Kengele iligonjwa kuashiria muda wa mapumzika umefika. Wote walitoka bustanini na kuendelea na ratiba ya shule.

*MWISHO*